Jikinge, jilinde, Chukua Tahadhari

Oktoba

# TIRA Updates 2025

Kwa Soko Salama la Bima

Toleo No.11 | Jarida la Mtandaoni | www.tira.go.tz



HALIUZWI

## JENGO LA TIRA BIMA HOUSE LAZINDULIWA RASMI DODOMA

**Wasiliana nasi** coi@tira.go.tz | **Au tupigie** +255 222 132 537 | **FB, IG, YT & LinkedIn:** //@tira_tz

# Yaliyomo



01





01 TIRA Imezindua Rasmi Jengo Jipya la Makao Makuu – "TIRA Bima House" Dodoma

03 TIRA Yatoa Tuzo Kutambua Mchango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Sekta ya Bima

06 TIRA Yazindua Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa Mwaka 2024

07 "TIRA Yaboresha Mifumo ya Kidigitali Sekta ya Bima" – Dkt. Baghayo Saqware

08 Huduma za Bima Zanzibar Ziendelee Kutolewa kwa Ubora - Mhe. Zena Said

10 TIRA Yawekea Mkazo Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote – Mafunzo Yafanyika Iringa

12 TIRA Yajadili mbinu za kukuza Sekta ya Bima Mkutano Mkuu wa CISNA 2025

13 TIRA Yawanoa Mawakili wa Serikali Sheria, Taratibu na Kanuni za Bima Zaelezwa

15 Mkutano wa Tatu wa Baraza la Nne la Watumishi wa TIRA Yaibua Chachu ya Ustawi Sekta ya Bima

17 Tunasimamia Msingi wa Maadili Kuwahudumia Wateja



**Jarida Hili limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma**

**Mhariri**
Hadija Maulid

**Waandishi**
Tabia Mchakama
Anna Massao

**Msanifu**
Abubakari W. Kafumba


TIRA Updates ni jarida la mtandaoni linaloandaliwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kupitia kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, likilenga kutoa taarifa muhimu, kuelimisha, na kuhamasisha umma kuhusu sekta ya bima nchini. Jarida hili limeandaliwa ili kufikia wadau mbalimbali wa sekta, wakiwemo mawakala wa bima, kampuni za bima, watoa huduma na watumiaji wa bima.

Jarida la TIRA Updates lina taarifa za matukio mbalimbali, ikijumuisha uzinduzi wa miradi mipya, semina, warsha za mafunzo, na mikutano muhimu inayofanyika ndani ya sekta ya bima.

Mbali na taarifa za matukio, TIRAUpdates lina makala maalumu zinazolenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima.

Aidha, toleo hili litaangazia matukio, habari na taarifa muhimu za mwezi Oktoba 2025.




Scan
Kusoma Kidijiti


Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe
**info@tira.go.tz**

Au
Piga simu bure **+255 222 132 537**

Tovuti yetu
**www.tira.go.tz**

# TIRA Imezindua Rasmi Jengo Jipya la Makao Makuu – "TIRA Bima House" Dodoma




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) tarehe 16 Oktoba 2025 imezindua rasmi Jengo jipya la Makao Makuu yake lililopo Njedengwa, Dodoma, linalojulikana kama TIRA Bima House. Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, wadau wa sekta ya bima, na wawakilishi wa taasisi za fedha. Tukio hilo limekuwa alama muhimu katika historia ya TIRA, likionesha hatua kubwa ya maendeleo katika kuboresha mazingira ya kazi na kuimarisha usimamizi wa sekta ya bima nchini.

Mgeni rasmi katika uzinduzi




huo alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Sera na Mipango Zanzibar, Mhe. Saada Mkuya Salum, ambaye katika hotuba yake alipongeza TIRA kwa hatua hiyo ya kihistoria na kusisitiza kuwa ujenzi wa jengo hilo ni kielelezo cha utekelezaji wa dhamira ya Serikali ya kuhamishia taasisi zake zote Dodoma na kuimarisha utendaji unaoendana na maendeleo ya uchumi wa kisasa.

Mhe. Mkuya pia alibainisha kuwa TIRA imeendelea kuwa chachu katika kukuza sekta ya bima nchini, na kuongeza kuwa Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kuhakikisha sekta hiyo inachangia ipasavyo katika pato la taifa na ustawi wa wananchi.

Pia aliitaka TIRA kuendelea na juhudi za kusimamia kwa weledi utekelezaji wa Sheria ya Bima, kuhakikisha kuwa watoa huduma wa bima wanazingatia kanuni na viwango vilivyowekwa, huku akisisitiza umuhimu wa kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya faida za bima na msisitizo kwa sekta ya bima kuwekeza zaidi katika ubunifu wa bidhaa zinazokidhi mahitaji ya Watanzania, hasa katika maeneo ya kilimo, afya, na majanga ya asili.

Kwa upande wake, Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, alieleza kuwa uzinduzi wa TIRA Bima House ni hatua muhimu kuelekea utoaji bora wa huduma, uwazi, na uwajibikaji katika kusimamia sekta ya bima.

Alisema jengo hilo jipya litakuwa kitovu cha ubunifu na usimamizi wa sekta, na kuahidi kwamba TIRA itaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na wadau wote wa bima ili kujenga sekta imara, jumuishi na endelevu kwa maendeleo ya taifa.

# TIRA Yatoa Tuzo Kutambua Mchango wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Sekta ya Bima



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetoa tuzo ya heshima kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutambua mchango wake katika Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, tuzo hiyo ilitolewa wakati wa Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima Tanzania uliofanyika Oktoba 16, 2025; TIRA Bima House Njedengwa, Dodoma.

Aidha, tuzo hiyo maalum ilipokelewa kwa niaba na Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo; Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar sasa (Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Ikulu - Zanzibar) Mhe. Dkt Saada Mkuya. Dkt. Samia amekuwa mstari wa mbele kwenye utekelezaji huo kutokana na matamko yake mbalimbali ambayo yanaonesha Serikali imejipanga katika kuhakikisha Sheria hiyo inatekelezwa. Julai 18, 2024, Songwe katika ziara yake Mhe. Rais alisema 'Ndugu zangu sisi ni wakulima wazuri, sisi wachimba madini wazuri; mvuno mmoja katika mwaka tenga fedha kidogo kanunue bima yako ya afya".

Kwa upande mwingine tuzo hizo za heshima pia zilitolewa kwa viongozi wengine mbalimbali kwa kuthamini mchango wao katika sekta ndogo ya bima wakiwemo Waziri wa Fedha (wakati huo), Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Mhe. Dkt. Saada Mkuya, Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar (wakati huo), CPA. Moremi Marwa, Mwenyekiti Bodi ya Taifa ya Bima na wajumbe wote, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dkt. Jim Yonaz, Kamishna wa Bima Dkt. Baghayo Saqware na Naibu Kamishna wa Bima, Bi. Khadija Said.












AIMP REPORT 20










TIRA

# TIRA Yazindua Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa Mwaka 2024




Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imezindua Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa mwaka 2024 iliyolenga kutoa taarifa ya maendeleo, changamoto na mwelekeo wa sekta ya bima nchini. Uzinduzi huo ulifanyika Oktoba 17, 2025; TIRA Bima House jijini Dodoma na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya bima, wakiwemo watoa huduma, makampuni ya bima na wawakilishi wa Serikali ambapo ilielezwa Mchango wa Bima katika pato la taifa nchini umeongezeka.


Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, alisema sekta ya bima inaendelea kukua kwa kasi ambapo mchango wa Bima katika pato la taifa umeongezeka hadi kufikia 2.08% mwaka 2024 kulinganisha na 2.01% mwaka 2023, kwa upande wa Wakata bima na wanafaika wa bima kuna ongezeko la 10.2%, Kutoka 23.5Mil hadi 25.9Mil sawa na asilimia 39.2 ukilinganisha na asilimia 37.7 mwaka 2023, ikimaanisha Wakatabima wam efikia 8.4Mil. na Wanufaikaji 17.5Mil.

Taarifa hiyo pia inatoa takwimu mbalimbali kuhusu Uendelezaji Soko la Bima, Masuala ya Usuluhishi wa Migogoro ya Bima (TIO), Madai ya Bima yaliyolipwa kwa kipindi husika, Watoa huduma waliofanya vizuri katika Soko ambao pia walitambuliwa na kupewa tuzo maalumu ili kutambua mchango wao.

Dkt. Saqware pia alieleza kuwepo kwa changamoto ya uelewa mdogo wa masuala ya bima ambapo Mamlaka imejipanga kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Bima ambapo wananchi wengi watafikiwa na kuongeza ujumuishi katika sekta, lakini pia maboresho ya huduma kwa njia za kidigitali yataongezeka kwa maendeleo ya Taasisi, sekta ya bima na wananchi kwa ujumla.

Mgeni rasmi katika Uzinduzi huo alikuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Sera na Mipango Zanzibar, Mhe. Saada Mkuya Salum ambaye aliipongeza TIRA kwa mafanikio hayo na kusisitiza uendelevu wa ushirikiano kutoka kwa Serikali na Sekta ya bima kwa maendeleo ya umma. Taarifa hiyo inapatikana katika tovuti ya TIRA ambayo ni www.tira.go.tz.

# "TIRA Yaboresha Mifumo ya Kidigitali Sekta ya Bima" – Dkt. Baghayo Saqware




Dodoma, 16 Oktoba 2025 — Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo Saqware, alisema sekta ya bima nchini imepiga hatua kubwa mwaka 2024, hususan kupitia maboresho ya mifumo ya kidigitali yanayolenga kuongeza ufanisi na uwazi katika usimamizi wa sekta hiyo. Akizungumza katika uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Soko la Bima kwa Mwaka 2024, uliofanyika katika jengo jipya la TIRA Bima House jijini Dodoma, Dkt. Saqware alisema:
"Tumeboresha mifumo ya kidigitali katika sekta ya bima ili kuongeza usambazaji na uandikishaji wa bima kwa haraka, ufanisi na uwazi. Lengo letu ni kuhakikisha huduma za bima zinapatikana kwa urahisi zaidi kwa Watanzania wote."

Aidha, Dkt. Saqware alitaja mafanikio sita yaliyopatikana katika sekta ya bima mwaka 2024, ikiwemo kuboresha mifumo ya kidigitali, utekelezaji wa Bima ya Safari kwa Wageni (Inbound Mandatory Travelling Insurance) Zanzibar, usimamizi wa utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote, uimarishaji wa usimamizi wa bima za lazima, utoaji wa miongozo mbalimbali ya sekta, pamoja na uanzishwaji wa konsotia mbili muhimu – ya Kilimo na ya Mafuta na Gesi.

Akizungumzia matarajio ya TIRA kwa miaka ijayo, Kamishna alisema Mamlaka inalenga kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa njia ya kidigitali, kuongeza wigo wa bima jumuishi kufikia asilimia 3 ifikapo mwaka 2030, na kuongeza wastani wa watumiaji wa bima kufikia asilimia 50 ifikapo mwaka 2050. Pia alieleza kuwa TIRA inaendelea na juhudi za marekebisho ya Sheria ya Bima, kutengeneza Sera ya Taifa ya Bima, na kuimarisha mikakati ya utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa bima.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya Bima ya Taifa, CPA Moremi Marwa, aliipongeza TIRA kwa mafanikio hayo na kueleza kuwa Bodi itaendelea kushirikiana na Mamlaka kutoa miongozo na maelekezo kulingana na sera na sheria zilizopo. Alisisitiza umuhimu wa uadilifu, ubora na uwazi katika utoaji wa huduma za bima, akisema hayo ndiyo misingi ya kuijenga sekta yenye uaminifu na uendelevu.

# Huduma za Bima Zanzibar Ziendelee Kutolewa kwa Ubora - Mhe. Zena Said



Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Mhandisi Zena Ahmed Said, ametoa wito huo kwa sekta ya bima nchini kuendelea kuwa wabunifu katika kuanzisha bidhaa mpya zitakazosaidia serikali kufikia lengo la kuchangia asilimia 3 ya Pato la Taifa ifikapo 2030.

Aliyasema hayo akiwa ni Mgeni Rasmi katika Maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Wateja 2025 TIRA, yaliyofanyika katika ofisi za Mamlaka zilizopo Unguja, visiwani Zanzibar. Aidha, Mhe. Zena alisema kampuni za bima zinapaswa kuboresha huduma, mazingira ya kazi na uwazi katika utoaji wa haki, "Tujitahidi kufanya inavyotakiwa na kutumia mbinu za haraka kutatua changamoto. Ubunifu kama bima ya ndoa ni mfano wa mwelekeo tunaoutaka," alisema.

Naye, Naibu Kamishna wa TIRA, Bi. Khadija I. Said, alisisitiza umuhimu wa huduma bora na lugha yenye staha kwa wateja, akisema Serikali inaendelea kuimarisha sekta hiyo kupitia bidhaa mpya zenye manufaa kijamii.

Kwa upande wake Meneja wa TIRA Kanda ya Zanzibar, Bw. Kurenje Mbura, alisema vituo 103 vya mauzo ya bima vimesajiliwa visiwani humo na kwamba TIRA inakamilisha mfumo utakaojumuisha bima katika masharti ya kupata kadi ya kutembea barabarani.

Kwa upande mwingine, Meneja wa Kitengo cha Ubora na Udhibiti Vihatarishi (QRM), Bw. Frank Fred Shangali alimalizia kwa kuhimiza kampuni za bima kuzingatia viwango vya ubora na mifumo imara ya mawasiliano ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa wateja.


WIKI YA HUDUMA
KWA WATEJA
2025


WIKI YA HUDUMA
KWA WATEJA
2025

# TIRA Yawekea Mkazo Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote – Mafunzo Yafanyika Iringa



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), kupitia Ofisi ya Kanda ya Kati, imetoa elimu kuhusu masuala muhimu ya bima, ikiwemo elimu juu ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura ya 161.

Elimu hiyo ilitolewa tarehe 24 Oktoba 2025 kwa Waganga Wafawidhi wa Wilaya kutoka katika Halmashauri ya Iringa. Aidha, lengo kuu la mafunzo hayo lilikuwa ni kuongeza uelewa kuhusu utekelezaji wa sheria hiyo, inayolenga kuhakikisha watanzania wote wanapata huduma bora, nafuu na endelevu za afya kupitia mfumo wa bima.

Kupitia mafunzo hayo, washiriki walijengewa uwezo wa kuelewa majukumu yao katika kufanikisha utekelezaji wa sheria hiyo ndani ya vituo vyao vya kutolea huduma za afya.

Kikao hicho pia kilihusisha takribani vituo vya afya 100 vilivyopo chini ya Halmashauri ya Iringa, ambapo washiriki walipata nafasi ya kujadili kwa kina namna bora ya kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya afya na sekta ya bima.

Aidha, vituo zaidi ya 180 vimeshasajiliwa rasmi na kutambuliwa na TIRA kwa ajili ya kutoa huduma chini ya mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Kupitia kampeni endelevu za utoaji elimu, TIRA Kanda ya Kati inaendelea kushirikiana na taasisi za umma na binafsi katika kuhamasisha uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa bima kama nyenzo ya msingi katika kuboresha ustawi wa wananchi, kuongeza usalama wa kifedha, na kuchochea ukuaji wa uchumi wa Taifa.





# TIRA Yajadili mbinu za kukuza Sekta ya Bima Mkutano Mkuu wa CISNA 2025




Mkutano Mkuu wa 48 wa Kamati ya Mamlaka ya Bima, Masoko ya Mitaji na Taasisi zisizo za Kibenki (CISNA) ambayo ni kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) umefanyika mjini Maun, Botswana, kuanzia tarehe 5 hadi 10 Oktoba 2025, ambapo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeshiriki.

TIRA ni mwanachama wa CISNA kutokana na wajibu wake wa kusimamia sekta ndogo ya bima nchini. Mkutano huu ulijumuisha vikao kazi vya kamati ndogo tatu — Capital Markets (CMS), Insurance and Retirement Funds, Medical Schemes and Intermediaries (IRMIS), na Microfinance and Financial Co-operatives (MiFFCO) — pamoja na kikao cha Governance Council na Baraza Kuu la CISNA (General Council Meeting). Moja ya jukumu la CISNA ni kuoanisha mifumo ya udhibiti na kukuza utekelezaji wa viwango vya kimataifa vya huduma za kifedha zisizo za kibenki.

CISNA inalenga kuhakikisha kwamba Mamlaka zote za udhibiti wa sekta za bima, masoko ya mitaji (securities), na taasisi zisizo za kibenki katika nchi wanachama wa SADC zinafanya kazi kwa viwango vinavyolingana na vinavyoendana na viwango vya kimataifa.

Aidha, kikao hicho kilifunguliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Botswana mnamo tarehe 7 Oktoba 2025, na kilihudhuriwa na wajumbe kutoka nchi wanachama wa SADC na wawakilishi wa taasisi za kikanda kama SADC Secretariat, ESAAMLG, CCBG, DFRC, na CoSSE. Miongoni mwa masuala yanayojadiliwa ni pamoja na marekebisho ya Kanuni za CISNA (CISNA Rules), ikiwemo pendekezo la nchi mwenyeji wa Sekretarieti kupewa kiti cha kudumu katika Baraza la Uongozi, uidhinishaji wa bajeti na taarifa za fedha, na utekelezaji wa Mkakati wa CISNA 2022–2026.

Tanzania iliwakilishwa na Kamishna wa Bima, Dkt. Baghayo A. Saqware, Mkurugenzi wa Mipango, Tafiti na Uendelezaji wa Soko, Bw. Samuel Mwiru, Mkurugenzi wa Leseni na Bima Mtawanyo Bw. Christopher Mapunda na Meneja wa Tathmini Bima na Uthabiti wa fedha Dkt. Peter Tengaa. Ushiriki wa TIRA katika mkutano huo ulikuwa sehemu ya jitihada za kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kubadilishana uzoefu wa kiudhibiti, na kukuza ufanisi wa sekta ya bima nchini Tanzania.

# TIRA Yawanoa Mawakili wa Serikali Sheria, Taratibu na Kanuni za Bima Zaelezwa




Katika kuhakikisha Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo ya Bima inafuatwa, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imetoa semina ya masuala ya bima kwa Mawakili wa Serikali nchini ili kuwaongezea uelewa katika kutekeleza majukumu yao. Semina hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Vizano Hotel, Oktoba 10, 2025 jijini Dodoma.

Aidha, mkutano huo ulifunguliwa rasmi na Mkurugenzi Msaidizi Uratibu kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bw. Ipyana Mlilo kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; ambapo aliipongeza TIRA kwa kuandaa mafunzo hayo yaliyolenga kujenga uwezo wa kisheria na kitaalamu kwa Mawakili yakisimamia Utekelezaji wa Malengo ya Dira 2050 na pia alitoa rai kwa Taasisi nyingine kuiga mfano wa Mamlaka kwa kutoa mafunzo kama hayo. Kwa upande wa Mamlaka; Bi. Margaret Mngumi, Msuluhishi wa Migogoro ya Bima kwa niaba ya Kamishna wa Bima alisema TIRA itaendelea kutoa Mafunzo yahusuyo bima ili kuhakikisha wanasheria wa Serikali na wadau wengine wanaongeza uelewa wa masuala ya bima.

Naye, Mkurugenzi wa Huduma za Sheria TIRA; Bw. Ponziano Lukosi alisema bima ni hitaji la msingi kwa kila Mwananchi na kusisitiza kuwa ni sekta ya muhimu sana hivyo mafunzo hayo yatasaidia Mawakili waweze kutoa msaada stahiki na kwa wakati kwa wananchi.

Aidha, Mawasilisho Matano yenye mada mbalimbali zikiwemo Sheria za Bima ya afya kwa wote, Uhusiano wa Mawakili wa Serikali na sekta ya bima, Sheria za Bima, Majukumu ya Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) ziliwasilishwa. Mada hizo zilitoa fursa ya maswali na majibu kuhusu masuala hayo ya bima lakini pia yaliongeza uhusiano imara kati ya TIRA na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maendeleo ya taifa letu.










SEMINA YA MASUALA YA BIMA KWA
MAWAKILI WA SERIKALI INAYOTOLEWA NA
MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA
TIRA

# Mkutano wa Tatu wa Baraza la Nne la Watumishi wa TIRA Yaibua Chachu ya Ustawi Sekta ya Bima



Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, na kila penye watu mshikamano ni nguzo kuu. Kauli hiyo imedhihirika katika Mkutano wa Tatu wa Baraza la Nne la Watumishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambapo watumishi hao walikutana kwa umoja wao kujadili masuala mbalimbali kwa maendeleo ya Taasisi hiyo, sekta ya bima na Taifa kwa ujumla.

Mkutano huo wa siku mbili ulifanyika tarehe 15 – 16 Oktoba katika ukumbi wa Mikutano wa Jengo la Ukaguzi, Dodoma.

Katika Hotuba yake wakati wa ufunguzi wa Mkutano huo Naibu Kamishna wa Bima na Makamu Mwenyekiti wa Baraza, Bi. Khadija Said alisisitiza Baraza la wafanyakazi lina nafasi ya kipekee katika kuhakikisha uwiano kati ya Usimamizi wa Taasisi na Watumishi lakini pia malengo ya pamoja katika ufanisi wa kazi yatakayowezesha umoja kwa ustawi wa watumishi, watoa huduma za bima na wananchi kwa ujumla.

Aidha, Bi. Khadija pia alieleza TIRA imeendelea kufanya mageuzi makubwa katika utendaji wake, ikiwemo kuimarisha mifumo ya kidijitali, ongezeko la bidhaa mpya katika soko, utoaji elimu kwa umma kuhusu masuala ya bima, na kuhakikisha watoa huduma za bima wanazingatia sheria, kanuni, na viwango bora vya utoaji huduma na kueleza mafanikio hayo yanatokana bidii, ubunifu na ushirikiano katika kazi unaofanywa na watumishi hao.

Kwa upande mwingine, Mkutano huo ulitoa fursa kwa watumishi kupewa elimu ya mtandao wa mawasiliano ya ndani, usalama katika TEHAMA, muundo wa Taasisi na elimu kuhusu afya ya akili. Watumishi pia walipata fursa ya majadiliano katika mada mbalimbali zilizowasilishwa ishara ya uwazi na ufanisi wa baraza hilo.








6. MAINTAIN YOUR EMOTIONAL RESERVES
6. MAINTAIN YOUR EMOTIONAL RESERVES


6. MAINTAIN YOUR EMOTIONAL RESERVES

# Tunasimamia Msingi wa Maadili Kuwahudumia Wateja



Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iliungana na Taasisi mbalimbali nchini kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja iliyofanyika wiki ya pili ya Oktoba 2025 ili kuhamasisha watumishi na wadau wote wa sekta ya bima kutambua umuhimu wa kutoa huduma bora na zenye ubora kwa wananchi, ikiwa ni sehemu ya juhudi endelevu za TIRA katika kuimarisha uhusiano kati ya watoa huduma za bima na wateja wao.

Kupitia maadhimisho hayo, TIRA ilionesha dhamira yake ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuzingatia maadili ya kitaaluma na misingi ya uwajibikaji.

Mamlaka imekuwa ikisisitiza matumizi ya teknolojia katika utoaji huduma, upatikanaji wa taarifa kwa uwazi, na kusikiliza maoni ya wananchi ili kuhakikisha huduma za bima zinabaki kuwa jumuishi, zenye kuaminika na zinazojibu mahitaji halisi ya jamii.


Si hivyo tu, kupitia kanda kumi za TIRA zilizopo Tanzania Bara na Visiwani TIRA imesogeza huduma za bima kwa wananchi ili waweze kujikinga na bima pamoja na mali zao.

Lakini pia Mamlaka inatoa taarifa mbalimbali kupitia mitandao ya kijamii mathalani kuhusu Sheria, Miongozo, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazoongoza soko la bima.

Mitandao hiyo ni pamoja na Mtandao wa Kijamii wa Instagram tira_tz, Thread tira_tz, lakini pia na Tovuti ya Mamlaka www.tira.go.tz.


# Vibango vya Matukio










# Majibu ya Maswali yako Kuhusu Bima

*Pata majibu ya maswali yanayoulizwa mara kwa mara*



**Bima ni nini?**

Bima ni mkataba wa kisheria kati ya pande mbili yaani kampuni ya bima na mtu binafsi, kikundi au kampuni (mbima), ambapo kampuni ya bima inaahidi kulipa fidia iwapo janga lililokatiwa bima litatokea na kusababisha hasara. Hivyo, bima ni nia ya kuhamishia majanga kwa kampuni za bima na kupata kinga dhidi ya majanga mbalimbali yasiyotarajiwa. Bima hukatwa kwa ajili ya kukinga majanga mbalimbali yanayotuzunguka kila siku.

## Majanga ni nini?

Ni hatari yeyote isiyotabirika inayoweza kusababisha upotevu wa fedha, maisha na mali. Hatari hizi zinaweza kutokea katika shughuli mbalimbali za kiuchumi na za kijamii kila siku. Hivyo, matukio kama ajali za vyombo vya usafiri, moto, mafuriko, magonjwa, ukame ni baadhi tu ya majanga yanayoweza kumkumba mwananchi.

## Bima ina umuhimu gani kwa mali na maisha ya mwananchi?

Bima ni muhimu kwani inahakikisha usalama wa kukabiliana na aina yoyote ya changamoto maishani. Bima ni sehemu muhimu sana katika mipango ya mwananchi katika uwekezaji wa kiuchumi na kijamii.

## Je, ni nani anastahili kuwa na Bima?

Bima ni nyenzo muhimu sana kwa kila mwananchi, hivyo hakuna anayebaguliwa ama kupewa kipaumbele sana katika kupata huduma za bima.

Hii ni kwa sababu kila mmoja kwa wakati fulani hukumbwa na janga aidha la kiuchumi (kupata hasara katika Biashara, kilimo, ufugaji n.k) na kijamii (yaani kuuguliwa, kufiwa na hata watoto kukosa ada na chakula n.k). Hivyo, kuzingatia aina hii ya uwezekano wa kupatwa majanga, jamii yote huhitaji bima za aina mbalimbali kulingana na uhitaji.

## Ni nani aliyepewa dhamana ya kutoa huduma za Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, Soko la Bima nchini linasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo hutoa leseni kwa kampuni za bima ambazo hubeba dhamana ya kutoa fidia kwa wananchi waliokata bima.

Pia, wananchi wanaweza kupata huduma za bima kupitia Washauri na Madalali wa Bima, Mawakala wa Bima kupitia Benki na Mawakala wa Bima waliosajiliwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria. Pia, kuna watoa huduma za bima wanaosajiliwa na Mamlaka kama Wakadiria Hasara, Wakaguzi Binafsi na Wakala wa Ufuatiliaji wa Fidia.

## Ni wakati gani Bima inahitajika?

Bima inahitajika mara tu unapokuwa hauna uhakika na uwezekano wa kuwa katika hali yako ya awali iwapo janga litakupata. Hivyo, ni vema ikafahamika kuwa bima hukatwa mapema ili kujikinga na janga kabla halijatokea. Iwapo itakatwa baada ya janga kutokea haitofaa kutoa fidia kwa janga lililopita.

## Je, ni lazima kuwa na Bima?

Kimsingi, mwananchi anawajibika kukinga mali na wapendwa wake kwa hiari yake kwa kuwakatia bima. Pamoja na hiari hiyo, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168 ya Mwaka 1973, iliyorekebishwa 2002 imewapasa wamiliki wa vombo vya moto wanaotumia barabara za umma kukata bima ndogo (Third Party Insurance) ili kumkinga mtu wa tatu dhidi ya majanga yanayosababishwa na vyombo vya moto.

## Je, ni nani mnufaika wa Bima?

Bima hunufaisha wamiliki wa bima au wakata (policyholders) na wahanga kulingana na aina

ya bima iliyokatwa na majanga yaliyosababisha hasara. Kwa mfano, Bima za Maisha na Bima za Afya hunufaisha mkataji bima ama wanufaika walioandikwa katika mkataba wa bima.

Kwa upande wa Bima za Muda Mfupi, mnufaika wa kwanza huwa ni mkata bima hususan kwenye bima za moto, kilimo, ajali, biashara, n.k. Bima ndogo (Third Party) hunufaisha moja kwa moja mtu wa tatu aliyesababishiwa janga iwe kuumizwa yeye mwenyewe ama kuharibiwa mali zake.

## Mkata bima ana wajibu katika suala zima la kupata huduma za Bima?

Ni kweli kuwa mkata bima anao wajibu katika hatua za kukata bima na wakati bima iko hai.

Wakati wa kukata bima atawaibika kutoa taarifa zote zinazohitajika kwa ukweli usiyo na shaka (bila kuongopa), kujaza fomu ya uhitaji wa bima na kutaja wanufaika (hii ni kwa Bima za Maisha na Bima za Afya), kuwa na nyaraka zote muhimu wakati wa ukataji bima kabla ya kuchukua mkataba wa bima; kufanya madai kwa mujibu wa masharti ya mkataba wa bima na kufuata mchakato wa madai.

## Je, pindi mkata bima anapopatwa na janga, ni wapi anatakiwa kutoa taarifa?

Pindi janga lililokatiwa bima linapotokea mkata bima mwenye mkataba wa bima anapaswa kutoa taarifa kwa kampuni ya bima iliyotoa kinga dhidi ya mali yake ili kuwezesha hatua zingine za fidia kuendelea. Utaoaji wa taarifa uzingatie taratibu zilizowekwa katika mkataba wa bima. Inashauriwa kutoa taarifa ndani ya masaa 24 baada ya janga kutokea.

Mhanga anaweza pia kutoa taarifa kwa wakala au dalali wa bima aliyemkatia bima. Lakini isisahaulike kuwa ni muhimu kutoa taarifa kwa vyombo vya usalama na ngazi mbalimbali za Serikali, kwa mfano: inapotokea ajali, mkata bima atoe taarifa Jeshi la Polisi - Usalama Barabarani au nyumba inapoungua ni vema kutoa taarifa Jeshi la Zima Moto na Uokoaji, kwa upande mwingine kuna Ofisi za Serikali za Mitaa, Vijiji na hata Kata.

Kutoa taarifa sehemu zote hizi hujenga msingi mzuri wa mkata bima kufidiwa bila mashaka ya tukio kwani linakuwa limehakikiwa na ngazi husika.

## Ni muda gani umewekwa kwa kampuni kushughulikia fidia kwa mhanga wa ajali au kuharibikiwa na mali iliyowekewa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Na. 10 ya Mwaka 2009, kampuni ya bima inapaswa kushughulikia madai ya wateja kwa muda mfupi kulingana na ukubwa wa janga na uthibitisho wa janga lenyewe kuwa halali. Baada ya kujiridhisha kuwa janga hilo ni sahihi na kutoa hati ya kukubali janga, kampuni itawajibika kutoa fidia kwa mteja ndani ya siku zisizozidi 45.

## Ni jinsi gani mteja anaweza kuwasilisha malalamiko kwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima?

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ndicho chombo cha Serikali kinachowajibika kumlinda mteja wa bima (mkata bima). Hivyo, ni sahihi kabisa

kwa mnufaika wa huduma za bima kuleta lalamiko lake dhidi ya huduma za bima anazopewa na kampuni za bima zilizosajiliwa na Mamlaka. Malalamiko yanaweza kuwasilishwa TIRA kupitia barua pepe au simu, kutegemea uko eneo gani nchini. Pia unaweza kuwasilisha malalamiko kupitia tovuti: www.tira.go.tz ambapo utajaza fomu ya malalamiko na kuiwasilisha.

## Je, kuna tofauti kati malalamiko ya Bima na migogoro ya Bima?

Malalamiko ya bima ni tofauti kigodo na migogoro ya bima, kwani malalaiko ya bima hutokana na huduma hafifu zinazotolewa na watoa huduma wa bima kwa wananchi waliosajiliwa na Mamlaka na mara nyingi aina hii ya malalamiko uhusisha wahanga wa ajali (third party) na haya huwasilishwa kwa Kamishna wa Bima kwa hatua stahiki.

Migogoro ya bima ni ile inayohusisha mteja kutokubaliana na kiwango cha fidia kutoka kwa kampuni ya bima. Migogoro hii hupelekwa kwenye Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) kwa hatua zaidi.

## Je, kuna Bima kwa ajili ya kilimo na mifugo?

Soko la Bima nchini linaendelea kukua kila siku. Aina mbalimbali za bima zinatolewa ikiwemo Bima za Kilimo naBima za Mifugo. Bima ya Kilimo hukatwa kwa ajili ya kukinga moto, mafuriko, ukame, wanyama na wadudu waharibifu. Kwa upande wa Bima ya Mifugo, hutolewa kwa ajili ya kukinga magonjwa, upotevu na vifo.

## Je, TIRA ina mifumo yoyote ambayo inaitumia katika usimamizi wa shughuli za Bima kwenye soko?

Ndiyo. Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ina mifumo mingi katika utoaji wa huduma za bima: Mafno: Mfumo wa TIRA-MIS unaotumika kukata bima na kuhakiki uhalali wa bima za vyombo vya moto na mali za mteja, mfumo mwingine ni Tanzania Import Insurance Portal (TIP) kwa ajili ya bima za mizigo kutoka nje ya nchi kwa njia meli (bahari) na dege (anga).

Pia mfumo wa Risk Based Supervision (RBS) kwa ajili ya upokeaji wa taarifa na uchambuzi wa viashiria vya majanga. Mifumo hii yote imeunganishwa na taasisi stahiki za Serikali pamoja na watoa huduma za bima.

## Je, ninaweza kuhakiki bima ya chombo cha moto na mali zangu?

Ndio, unaweza kuhakiki bima yako kwa kutumia mfumo wa TIRA-MIS.

## Je, Kuna Bima kwa ajili watu wa kipato cha chini?

Ndio. Ipo bima kwa ajili ya watu wa kipato cha chini, bima hii hufahamika kama "'microinsurance'. Ni bima ndogo ambayo ni kwa ajili ya kumkinga mtu asiyeweza kuingia kwenye utaratibu wa bima yenye gharama kubwa kutokana na kiwango cha fedha anachokipata.

Mfano kwa wale wanaofanya shughuli za uJulainga, mama/baba lishe, na wengine wenye biashara ndogo ndogo. Bima hizi hulipa fidia endapo mbima atapata hasara kwenye biashara yake aliyoikatia bima.



# TIRA & 2025


**Mamlaka ya Usimamizi wa Bima**
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
PSSSF HOUSE, 5th Floor, Makole Street, P.O. Box 2987
DODOMA, Tanzania.

coi@tira.go.tz
+255 26 2321180
+255 0222135137
+255 26 2321180

**FB, IG, X:** //@tira_tz
www.tira.go.tz